

GABRIEL RUHUMBIKA: *JANGA SUGU LA WAZAWA* (2002). UCHAMBUZI NA UHAKIKI

JOHN P. MBONDE

1. Utangulizi: Mwandishi na Uandishi wake

Gabriel Ruhumbika aliyezaliwa mwaka 1938 kisiwani Ukerewe ni miongoni mwa wanafashihi waliokubuhu katika fani ya riwaya za Kiswahili. Riwaya yake nyingine ni ile miongoni mwa vitabu teule (1997-2001) kwa ajili ya kutahinia wanafunzi wa shule za sekondari kidato cha sita iitwayo *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992). Vitabu vingine alivyopata kuandika ni pamoja na *Uwike Usiwike Kutakucha* (mkusanyiko wa hadithi fupi; 1978)¹; *Afrika Inakwenda Kombo* (tafsiri; 1976); *Viumbe Waliolaaniwa* (tafsiri; 1978). Pia ametoa mkusanyiko wa hadithi fupi za wanafunzi wake uitwao *Parapanda* (1974)², na mkusanyiko wa insha za kisiasa (1974). Aidha, amehandika riwaya moja kwa lugha ya Kiingereza iitwayo *Village in Uhuru* (1969). Sasa ametuletea riwaya hii ya aina yake *Janga Sugu la Wazawa* (2002).

Kufuatana na habari tulizo nazo, Gabriel Ruhumbika alipata shahada ya kwanza (*B.A.Hons. English*) ya Chuo Kikuu cha London mwaka 1964 kama mwanafunzi wa nje wa Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda. Halafu akasoma katika Chuo Kikuu cha Sorbonne, Paris, Ufaransa, na kupata shahada ya tatu (Ph.D.) mwaka 1969. Alikuwa mhadhiri na profesa wa fasihi katika Idara ya Fasihi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa muda wa miaka kumi na mitano (1970-1985). Halafu alikwenda Marekani na kufundisha katika Chuo Kikuu cha Hampton, Virginia, akiwa profesa wa Kiingereza (1985-1992). Kuanzia mwezi Septemba mwaka 1992 amekuwa Profesa wa Fasihi Linganishi (*Comparative Literature*) katika Chuo Kikuu cha Georgia mjini Athens, Marekani. Aidha, amepata kutembelea na kutoa mihadhara kwenye vyuo mbalimbali nchini Marekani na barani Ulaya.

2. Muhtasari: Msuko na wahusika

Riwaya ya *Janga Sugu la Wazawa* (JSW), ingawa linazungumzia mila na desturi za Wakere-we na mfululizo wa mikasa iliyoandama familia ya Mzee Ninalwo na wanawe, inaihusu jamii nzima ya Tanzania. Mwandishi anabainisha kwamba hatimaye kila mahali kote nchini wananchi wakaogopa zaidi hili janga sugu la jamii yao kuliko kitu kingine chochote hapa duniani. Lakini je, hilo janga sugu la jamii ni lipi? Mwandishi anawaweka wasomaji katika

¹ Ni mkusanyiko wa hadithi fupi nne: *Bunge la Wachawi, Kisa cha Mlevi wa Gongo na Mchwa, Mizimu Kushtakiwa Mahakamani na Dua la Kuku lilivyompata mwewe*. Kitabu hicho pamoja na vingine vimeorodheshwa kwenye marejeo. Tz. hapo.

² Mojawapo ya hizi hadithi fupi iitwayo *Wali wa Ndevu* iliandikwa na 'G. Tilumanywa' ambaye ni jina la kiuandishi la Ruhumbika mwenyewe. Tz. Bertoncini-Zúbková 1989: 98.

taharuki kubwa hadi mwishoni mwa kitabu ndipo anaposema: “[...] *janga sugu la wazawa wa nchi zetu: Ushirikina na madhara yake yote*” (JSW: 192).

Kufuatana na riwaya hii, hili janga sugu la mauaji yanayotokana na ushirikina lilikua na kukomaa kote Tanzania ili kufanikisha miradi mikubwa mikubwa ya wakubwa na matajiri iliyotambikiwa binadamu na kuwekewa mawe ya misingi na wakuu fulani nchini:

Kufuatana na mauaji ya namna hiyo kukubalika hadi kwa wakuu wa nchi wenye-we, polisi na vyombo vingine ya usalama nchini vikawa haviyashughulikii tena. Kwa hiyo, waganga wa kienyeji na washirikina wa kila aina wakawa huru kufanya maovu ya biashara yao wapendavyo. Pakaanzishwa vyuo vya ushirikina, makanisa ya ushirikina, mahekalu ya ushirikina, dini za ushirikina...” (JSW: 186f.)

Baada ya kutambulisha hili janga sugu la wazawa ni lipi, tutaangalia muundo wa riwaya yenyewe. Riwaya hii imegawanyika katika sehemu nne yaani sehemu ya kwanza hadi ya tatu ikifuatwa na sehemu ya mwisho iitwayo ‘Hitimisho’. Sehemu tatu za mwanzo zimegawanyika katika sura kumi.

Tofauti na wahusika katika riwaya nyingi, wahusika wengi katika *Janga Sugu la Wazawa* wamekuwa ni wanafamilia wa familia moja: wazazi na watoto wao pamoja na wakwe zao wa kiume na wa kike. Majina yao yana maana maalumu miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, maana ya jina la Ninalwo itaelezwa hapo baadaye. Ni wahusika wa marika mbalimbali, lakini wenye kuamini na kuzingatia mila na desturi zao za jadi. Katika aya zitakazofuata, tutaambulisha wahusika wakuu pamoja na wahusika wengine.

Bugonoka Nseko ambaye ni kitindamimba kati ya watoto kumi na mbili wa Ninalwo na Nakazenze ni mhusika mkuu wa riwaya hii. Anasawiriwa kama mwanamke mwenye upendo mkubwa kwa ndugu zake. Pia inadhihirika kuwa Bugonoka ni mwanamke jasiri anapopambana kwa ukakamavu na Padri Joni na kumshinda wakati padri mzembe huyo alipotaka kumbaka.

Huyu Padre Alhaji Sheikh Joni Juma Profesa Simba-Mbiti ambaye ni mganga wa kienyeji ni mhusika mkuu mwingine. Tabia yake yajionyesha tayari katika jina lake refu ajabu. Ni padri wa kanisa la katoliki la Nyamazugilo. Padri Joni anasawiriwa kama mpenda ngono ambaye ufuska wake hauna kifani. Tunaelezwa kuwa anataka kumbaka Bugonoka. Ingawa mapadri wa kanisa katoliki hupaswa kuzingatia useja kwa dhati, Padri Joni anajitosa kwenye umalaya. Mwishowe makao makuu ya kanisa ya Vatikani yanafedheheshwa mno na kwa hivyo kulazimika kumfukuza upadri ili kulinda hadhi ya kanisa. Kutokana na kuchanganyikiwa, aliye kuwa padri anajipachika majina ya vyeo vingi kama alivyofanya dikteta wa kifashisti Idi Amin wa Uganda. Anajipachika hadhi ya Alhaji; pia kujitia kuwa ni Sheikh; badala ya kuendelea na jina lake la kikristo, Joni, anajisilimu na kuitwa Juma. Anajifanya kuwa ni Profesa ili kuwadanganya wagonjwa na watu wenye matatizo aweze kuwarubuni kwa madawa na mbinu zake za unabii wa uongo. Simba-Mbiti ni jina la ubabe katika uganga wa kienyeji. Aghalabu, ni katili kama simba hata alimuua Bugonoka ili kulipiza kisasi cha kukataliwa tendo la kujamii naye kwa nguvu. Ni mshirikina kwa kutumia viungo vya miili ya binadamu katika uganga wake. Hali kadhalika, anaisaliti familia ya mzee Makene kwa kuwapa

JANGA SUGU LA WAZAWA: UCHAMBUZI NA UHAKIKI

dawa ya kuwaangamiza huku akijidai kuwa ni rafiki yao. Ni mhusika anayesawiriwa kama mnaufiki mkubwa.

Wahusika wengine wanaowazunguka wahusika wakuu hao wawili watatambulishwa kwa ufupi hapo chini.

Ninalwo ni baba wa watoto kumi na mbili. Jina Ninalwo kwa Kikerewe lina maana kuwa ‘mauti tunaishi nayo’. Ninalwo anasawiriwa kama ni hodari sana wa kuvua na ana utajiri mkubwa wa mifugo. Pia ni mkuu wa kijiji na mshauri mkuu.

Nakazenze ni mke wa Ninalwo, hodari wa kulima na mwenye mkono mzuri wa kupika pombe. Akina mama wengine pale kijijini wanamjali na kumheshimu kama mama na bibi yao. Ni mkarimu na mcheshi, hivyo anapendwa sana na wanakijiji.

Wahusika wengine ambao hatutawatambulisha kwa urefu ni Mkaya, Tekeleye, Nagona, Mukula, Nakazenze-Mdogo, Nabina (mabinti wa Ninalwo), Magayane, Mwendante, Mtilya, Ninalwo-Mdogo, Nagabona (watoto wa kiume wa Ninalwo), Bwere (mume wa Mkaya), na Matondane (mtoto wa Magayana).

Halafu kuna Katekista Mzee Yosefu ambaye ni mwalimu wa dini wa Bugonoka hadi anapofika kubatizwa. Aidha, katekista huyo anaishi jirani nao. Mhusika mwingine, Fratera Joni, ni kijana wa Kisukuma ambaye ni msemnari wa Seminari Kuu ya Kipalapala Tabora. Fratera Joni anapata kuwa mgeni wa heshima kwenye sherehe nyumbani kwa mzee Ninalwo wakati wa ubatizo wa Mazula na mama yake Bugonoka. Bugonoka anachagua jina la Kikristo Zina-ida ambalo ni jina la mke wa Katekista Mzee Yosefu.

Kwa upande mwingine, mhusika mwingine ni Maimuna, mwanamke wa Dakar, Senegal, ambaye ni mfanyabiashara mashuhuri wa madini na vyakula. Amerithi utajiri mkubwa wa maduka kutoka kwa babake. Aliolewa kwanza na mwanaume wa Kisenegal na kuzaa naye watoto wawili. Kutokana na ujasiri wake, alimfukuza mume wake wa kwanza kwa sababu ya umalaya wake wa kutembea na wanawake wengine. Hatimaye aliolewa na Padri Joni. Hiyo ndiyo sababu ya kusilimiwa kwa Padri Joni kwa vile Maimuna ni Mwisalamu. Walibahatika kuwa na watoto watano. Maimuna anasawiriwa kama ni mwanamke mrembo ambaye urembo wake hauonyeshi hata dalili za uzee. Vilevile ni jasiri, hata anampa onyo kali mume wake wa pili, Padri Joni, kwa ufuska. Ingawa ana upendo mkubwa kwa waume zake hata kuwaamini kuendesha miradi yake ya uchumi, lakini wanaume hao wanahujumu na kudhulumu mali yake. Maimuna ana bidii katika kazi licha ya kuwa tajiri, lakini anafanya kazi nyingi za nyumbani kwa mikono yake mwenyewe pamoja na wafanyakazi aliowaajiri. Ni dhahiri kwamba mhusika Maimuna anafanana kitabia kwa ujasiri na Bugonoka.

Si jambo la kushangazwa kuona kuwa majina ya wahusika katika *Janga Sugu la Wazawa* yana mwingilianomatini (*intertextuality*) na riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. Ntulanalwo na Bulihwali* kilichoandikwa na Aniceti Kitereza mwaka 1945 (Kitereza 1980), kwa sababu Gabriel Ruhumbika alipata kukitafsiri kutoka Kikerewe kwa Kiingereza hata kabla hakijachapishwa kwa Kiswahili. Tafsiri hiyo ya Kiingereza hatimaye ilichapishwa

mwaka 2002 (Kitereza 2002). Majina hayo ya wahusika yanaelezea tunu na utamaduni wa Wakerewe.

3. Dhamira

Katika sehemu hii tutachambua dhamira zinazojitokeza zaidi katika riwaya hii:

- | | |
|-------------------------|------------------------------------|
| 1. Uchawi na Ushirikina | 5. Ukale na Usasa |
| 2. Dini | 6. Siasa na Uchumi |
| 3. Elimu | 7. Uongozi |
| 4. Utamaduni | 8. Nafasi ya Mwanamke katika Jamii |

Kuna dhamira nyingine ambazo zimejitokeza katika riwaya hii ambazo kwa namna moja au nyingine zinazizunguka hizi zilizoordheshwa hapa juu.

3.1. Uchawi na Ushirikina

Miongoni mwa mikasa mikubwa inayoikumba Afrika ni tishio la hisia za uchawi na ushirikina ambazo mwandishi Ruhumbika amezibandika kuwa ndizo chanzo kikuu cha janga sugu la wazawa. Dhamira hii imepewa kipaumbele katika riwaya hii. Kwa mfano, katika sura ya pili tunaelezwa: *“Waliamini kwamba kutoka kwenye msiba na kwenda kwenye hatari ya kifo usiku ni kujitafutia mkosi.”* (JSW: 27). Katika sura hiyo hiyo tunaambiwa kwamba Mzee Ninalwo baada ya kuandamwa na mfululizo wa vifo vya watoto wake anaondoka na watoto wa kiume ili kutembea humu duniani kwa shabaha ya kujua chanzo cha janga lililowaangukia (tz. JSW: 36). Safari hiyo inaashiria jinsi vipi imani za uchawi na ushirikina zinavyotawala karibu jamii nzima ya Waafrika. Halafu tunaelezwa: *“Wakatokomea Usukumani kote na kuona waganga wenye kila aina ya kago na zindiko za kukinga uzima wa binadamu.”* (JSW: 42).

Nao waganga wa kienyeji wamechukulia hofu hii ya jamii dhidi ya uchawi na ushirikina kama mradi wao wa kuchumia utajiri. Ndiyo sababu waganga hao hujipachika majina kuwa ni maprofesa. Matokeo yake tunaisoma katika sehemu ya mwisho (‘Hitimisho’):

“Biashara ya ushirikina ikaongoza katika kutajirisha watu kwenye uchumi wa nchi, bali tu wanaotajirishwa na hiyo biashara ya kutisha wakiwa ni wale wachache wanaoiendesha pamoja na wafadhili wao, huku kwa umma wa wana-nchi kila mahali biashara hiyo ya kutisha ikawa pia ndiyo sasa chanzo kikubwa cha umaskini wao na ugumu wa maisha yao, licha ya kuwa tishio kubwa kuliko yote kwa uhai wao na usalama wa jamii yao.” (JSW: 187)

Biashara ya ushirikina na uchawi imeleta mitafaruku na kusambaratisha mifumo mbalimbali ya jamii duniani na hasa katika bara la Afrika. Kwa maneno mengine, hicho ndicho ‘Janga Sugu la Wazawa’. Ingawa waandishi wengi hugusia athari za ushirikina na uchawi, bado ha-pajatafutiwa ufumbuzi wa kudumu dhidi ya janga hilo.

3.2. Dini

Dhamira hii imejitokeza mahali pengi katika riwaya, hususan dini za jadi, Ukristo na Uislamu. MATHALANI, matambiko, taratibu za mazishi, ndoa na imani zilizotawala mifumo ya maisha ya kila siku ya Wakerewe viliegemea kwenye dini ya jadi. Mgongano baina ya dini ya jadi na Ukristo ulioletwa na mamisionari unasawiriwa katika dondoo lifuatalo:

Ninalwo, na kadhalika baba yake Magayane, pamoja na wazee wengine wa kabila lake hawakupeleka watoto wao shule kwa sababu ya hiyo dini ya Wazungu. Huko Ukerewe Wazungu walijenga shule yao Kagunguli, karibu na Bukindo, Ikulu ya watemi wa nchi tangu enzi ya Wajerumani. Wakerewe asilia kama Mzee Ninalwo waliendelea kuisusia shule hiyo kwa sababu mtu alipoandikisha mtoto wake shule, mapadre wa Kizungu walitaka mtoto, pamoja na baba yake wabatizwe. Masharti ya baba yake kubatizwa ilikuwa ni kufukuza wake zake wote na kubakia na mmoja tu, kama alikuwa na wake wengi. Mke wake mkubwa wa kwanza tu ndiye angebaki. Zaidi ya hapo, mtu alitakiwa achome moto vifaa vyake vyote vya kutolea sadaka na kusalia kufuatana na dini ya asili ya watu wake na mababu zao. "Tunakubali hawa Wazungu walitushinda na kututawala," Mzee Ninalwo na wazee wa Kikerewe wenzake walisema, "lakini ndiyo tukubali pia watuvunjie miji yetu na kutwamuru tuoe wake wangapi na tuoe mke gani? Tuchome vifaa vya imani ya mababu zetu, ati ni imani ya 'kishenzi'! Imani ya Mungu wa uwongo, kama kwamba wao waliumbwa na Mungu tofauti na Muumba wa kila kitu ulimwenguni!" (JSW: 75)

Wakati wamekabiliwa na dhoruba, Mazula alikuwa amerithishwa jadi ya kumtambikia Mungu wa Ziwa la Nyanza (Victoria), alimwuliza mama yake: "Mama, labda nitoe sadaka?" (JSW: 31.) Mama yake akamhimiza atoe sadaka mara moja. Mazula akamtambikia kwa sala maalumu:

"We Mugasa! Mungu wa maji yote ulimwenguni, turuhusu tuwasili salama Ngoma, tunapokwenda kumlilia ndugu yetu aliyetuacha, kama binadamu wanavyopaswa kufanya mmoja wao wampendaye anapofariki." (JSW)

Aidha, tunaelezwa kuwa Mazula na Bugonoka wanabatizwa na kuwa wakristu wa Kanisa Katoliki (tz. JSW: 76f.). Hali kadhalika katika sura ya saba tunaambiwa: "Padre Joni akasilimu, kwa jina la Isa, na kumwoa mpenzi wake Maimuna" (JSW: 127).

3.3. Elimu

Kutoka mwanzo wa riwaya hii dhamira ya elimu imetiliwa mkazo wa pekee. Kwa kadiri ya elimu dunia, tunamwona Mzee Ninalwo anawapa wanawe maadili mema ya jinsi ya kuishi na watu na umuhimu wa kufanya kazi. Hali kadhalika, anamwandaa Bugonoka kutekeleza majukumu ya kijadi:

"Bugonoka, mdogo mtu, ndiye alikuwa awe binti mdogo wa kulisha jadi maharusi, msindikizaji mdogo wa bibi harusi atakayeungana na msindikizaji mkubwa, shangazi yao." (JSW: 6)

Katika sura ya tano (tz. JSW: 80f.) tunaelezwa juu ya masomo ya watu wazima. Mazula anamweleza mamake, Bugonoka, "Isitoshe ningefurahi tu kuona unajua kusoma na kuandika." Azma hiyo inatekelezwa na yeye Mazula kwa kumfundisha mama yake kusoma na kuandika. Na wazazi wa Bugonoka wanaelezea kuridhika kwao:

“Lakini mimi pia nimejionea Bugonoka wetu akisoma barua bila kusita, kama anasimulia tu, kama naye alisoma kwenye hayo mashule ya Wazungu.” (JSW: 81)

Aidha, tunaelezwa kuwa Bugonoka alijitahidi kumsomesha mwanawe, David Mabula hadi Chuo Kikuu cha Makerere alikojiipatia shahada. Baadaye alifanikiwa kupata shahada ya juu kabisa (Ph.D.) (tz. JSW: 112) huko kwenye Chuo Kikuu cha Havard, Marekani, na hata akawa profesa. Na mke wake Profesa Mabula, Angela, alijiendeleza katika elimu kuanzia ngazi ya ualimu hadi naye akaingia Chuo Kikuu na kupata shahada ya kwanza na baadaye shahada ya pili (M.A.) (tz. JSW: 116).

Kwa maneno mengine, riwaya hii inatilia maanani sana kwamba elimu ni ufunguo wa maendeleo kwa binadamu wa jinsia zote, wake kwa waume, watoto kwa wazee. Walakini, ‘Elimu nyingi huondoa maarifa’ ni usemi uliomtia kiburi Padre Alhaji Sheikh Joni Juma Profesa Simba-Mbiti, kwamba watoto wa Makene wasingeweza kumwua mbele ya kadamnasi ya umati wa watu waliokusanyika ili kushuhudia yale yatakayopata baada ya miaka yake mingi ya kazi hiyo ya kuchezea akili za binadamu wenzake: *“Hii ndiyo hasara ya kutokuwa na elimu.”* (JSW: 173). Lakini aliyotendewa hadi kuutoa uhai wake yalibainisha ukweli kwamba elimu ni nywele kila mmoja anazo zake. Kwa kweli, tamaa ya fedha inakwenda sambamba na wivu kumepolekea kuwa na janga sugu la wazawa.

3.4. Utamaduni

Utamaduni unahusisha masuala mengi yakiwa ni mfumo wa maisha, mila na desturi, mavazi, nyimbo, vyakula, ujenzi wa makazi, uzalishaji mali, malezi ya watoto, ndoa, vifo na mazishi, urithishaji wa kizazi hadi kizazi, na kadhalika.

Katika riwaya hii utamaduni wa Wakerewe umejitokeza zaidi, ikiwa ni pamoja na wa Kisukuma kwa upande mwingine. Kuna mifano mingi sana inayodhihirisha waziwazi jinsi wahu-sika wanavyoathiriwa na tamaduni zao. Kwa mfano, katika sura ya kwanza tunasoma:

“Magayane, alikuwa ni mvuvi hodari aliyenunua ng’ombe na mbuzi kwa biashara ya samaki. Na wanawe wote walifuata jadi ya baba na babu yao ya kuchuma kwa kuvua na kuuza samaki.” (JSW: 5)

Halafu (tz. hapo juu) tunasoma:

“Bugonoka, mdogo mtu, ndiye alikuwa awe binti mdogo wa ‘kulisha jadi’ maharusi...” (JSW: 6).

Hali kadhalika tunaona jinsi umuhimu wa tambiko ulivyotawala jamii:

“Alikuwa amerithishwa jadi ya kutambikia Mungu wa Ziwa Victoria Nyanza na maji yote ulimwenguni.” (JSW: 31)

3.5. Ukale na Usasa

Dhamira ya ukale na usasa ambayo ndiyo dhamira kuu ya riwaya nyingi za waandishi wa Kiafrika pia imesawiriwa katika riwaya hii. Katika sura ya kwanza tunaelezwa kuwa mji wa Mzee Ninalwo ulikuwa umejengwa na kujengeka hadi kunguruma. Nyumba yake ilikuwa

JANGA SUGU LA WAZAWA: UCHAMBUZI NA UHAKIKI

“[...] ilipigwa lipu nje na ndani na kuzekwa kwa majani adimu ya olumbwe, yanayong’aa kuliko hata paa la bati. Wakerewe walidai kwamba yanadumu kizazi kizima.” (JSW: 4)

Hapo tunaweza kuchambua kwamba mabati yanawakilisha usasa na majani adimu ya *olumbwe* yanawakilisha ukale.

Tunapoambiwa juu ya uvuvi wa samaki kuwa ni jadi ya baba na babu (tz. JSW: 5) humaanisha ukale kwa kutumia mitego ya *lubigo*, lakini katika sura ya tisa (tz. JSW: 155) tunaelezwa juu ya uvuvi wa kisasa wa kutumbia boti zenye injini; hali kadhalika katika sura ya kumi (tz. JSW: 162) tunaelezwa juu ya vyombo vya kisasa vya kusafiria majini ikiwa ni pamoja na spidiboti, mashua ndogo za kisasa dhidi ya mitumbwi.

Katika sura ya kwanza tunamsikia Mzee Ninalwo akiwapa wasia wanawe kutokana na mang’amuzi yake:

“Kama makadirio yake yalikuwa sawa, mwaka huo mwanawe huyo wa mwisho alipofikisha miaka kumi, yeye alifikisha miaka sitini na mbili. Aliwasimulia wanawe kwamba alimwoa mkewe, Nakazenze, alipokuwa na umri wa miaka kumi na minane, wakati mke wake alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano.” (JSW: 7)

Kauli hiyo inatoa onyo kwa vijana kuacha kuyapapatikia malimwengu mageuzi yanapovuma kama upepo wa kisulisuli na kasi ya utandawazi.

3.6. Siasa na Uchumi

Siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi wake, utamaduni, na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo; mfumo wa mawazo ya-ongozayo utawala wa serikali ya nchi; utaratibu wa utekelezaji au uendeshaji wa jambo kwa kutumia busara na hekima ili kufikia lengo linalotarajiwa (tz. KKS 1981: 259).

Kwa mantiki hiyo, Wakerewe walikuwa na siasa yao katika uvuvi, usafiri katika ziwa, wakati wa misiba, uzazi, malezi, na kadhalika Kwa mfano, upo utaratibu wa kuwaita watoto kwa majina ya mababu, mabibi, au yale yenye maana maalum ya matukio (tz. JSW: 5-8 na pengi-nepo).

Hali kadhalika, suala la uchumi linasawiriwa katika riwaya hii. Katika sura ya kwanza tunasoma:

Mzee Ninalwo, kama kabla yake alivyokuwa baba yake marehemu Magayane, alikuwa ni mvuvi hodari aliyenunua ng’ombe na mbuzi kwa biashara ya samaki. Na wanawe wote wakafuata jadi ya baba na babu yao ya kuchuma kwa kuvua na kuuza samaki.” (JSW: 5)

Aidha, katika sura ya nne tunaelezwa:

“Mtemi wa Ukerewe alikuwa anahimiza watu wake kupanua kilimo cha pamba na mpunga, na akahamasisha kwa kumpa kila mwenye nguvu hiyo ardhi mpya anayofyeka iwe yake na wanawe milele.” (JSW: 61)

Aghalabu, katika sura ya sita tunaelezwa kuhusu vuguvugu la harakari za kudai uhuru:

“Hapo pia ndipo palipokuwa na ofisi ya chama cha TANU. Tangu miaka kadha sasa chama hicho cha kupigania uhuru wa Mwafrika wa Tanganyika, ambao ulikuwa tayari unanukia, kilikwisha fungua ofisi hapo iliyokuwa ina pia tawi la Umoja wa Wanawake wa TANU. Bugonoka naye alikuwa tayari ni mwanachama wa U.W.T.” (JSW: 105)

3.7. Uongozi

Katika riwaya hii, dhana ya uongozi inasawiriwa kwenye viwango tofauti: kiwango cha kifamilia, kiwango cha kitaifa, na kiwango cha dini.

Kwenye kiwango cha kifamilia, tunaiona dhana ya uongozi bora kwa wazazi Mzee Ninalwo na Bibi Nakazenze, jinsi walivyowalea watoto na wajukuu wao, na jinsi walivyothamaniwa na ndugu majirani hata nyumbani kwao pakawa ni darasa la malezi bora.

“[...] walikuwa ni wazee wapole sana lakini pia ni wazazi wenye nidhamu, wasioruhusu kamwe mtoto kudekezwa [...] na ndiyo sababu kubwa ndugu zao na jamaa zao wengi hivyo waliwaleta watoto wao kulelewa hapo.” (JSW: 18)

Hawa walikuwa ni mfano mzuri wa kuigwa katika uongozi bora katika jamii. Wazee hao hawakupata kusoma darasani, lakini walijaa hekima na busara kubwa kuwashinda wale waliohitimu elimu ya vyuo vikuu. Katika sura ya kwanza tunaambiwa:

“Mzee Ninalwo alikuwa ni mmoja wa wazee mashuhuri wa kijiji chake cha Ngoma na mshauri mkuu wa Omukungu wao, mkuu wa kijiji.” (JSW: 7)

Katika riwaya hii dhamira ya uongozi bora inadhihirishwa bayana kwa azimio la pamoja la viongozi wa Afrika walipopanga mikakati ya mbinu za kudumu za kupiga vita ushirikina Barani Afrika (tz. JSW: 189-193). Viongozi hao wanaamini kuwa umoja ni nguvu, na kwa mshikamano huo vita dhidi ya mauaji ya kishirikina yatatokomezwa na hatimaye kufaulu kujenga jamii mpya. Mshikamano huo wa viongozi na wananchi utawawezesha kuitafutia jamii yao maendeleo na fanaka, huku wakifurahia maisha ya uzima na usalama.

Kwenye kiwango cha dini, inasawiriwa jinsi Padre Joni akiwa ni kiongozi wa dini anavyokuwa na tabia chafu kwa kuwa na mmomonyoko wa maadili ya useja. Kutokana na utovu wa nidhamu, Padre Joni anapokuwa kwenye masomo huko Roma analisaliti kanisa lake na akawa anasutwa:

“Ikawa ni kama hakuja huko kusomea mambo ya dini yake bali kilichomleta ni kulala na wanawake wa Kizungu, tangu masista watawa hadi malaya kwenye madangaro [...]” (JSW: 122)

Kwa kukosa msimamo wa imani ya dhati ya dini yake, padre Joni akaamua kusilimu wakati akiwa huko Senegal na kumwoa mwanamke wa Kiislamu, Maimuna ambaye alikuwa tajiri mkubwa mjini Dakar. Akaponda mali ya huyo mkewe kwa kutembea na dogodogo wa hapo Medina mjini Dakar. Padre Joni alikuwa sasa mashuhuri kama Alhaji Sheikh Isa Juma. Kutokana na tabia yake mbaya alifarakana na Maimuna, lakini alifaulu kutoroka na pesa nyingi za mwanamke huyo na kurejea Tanzania na kufanya maskani yake Iganzo Mwanza akiwa mganga akijulikana kwa jina la Profesa Simba-Mbiti. Na hatima yake, kwa matendo yake maovu ya kuendeleza mauaji ya watu lukuki, Padre Alhaji Sheikh Joni Juma Profesa Simba-

JANGA SUGU LA WAZAWA: UCHAMBUZI NA UHAKIKI

Mbiti aliuawa kwa kusulibiwa kwenye mti uitwao mbulumatale visiwani Ukerewe kwa kuto-bolewa kwa mpini wa jembe toka utosini kupitia tumboni hadi chini ardhini huku watu waliomshabikia umashuhuri wa uganga wake wakimwangalia akiuwa na baadaye hao, wa-kaenda zao.

“Umambo uliomwua mganga wa kienyeji mashuhuri kuliko wote nchini Tanzania na nchi jirani ukaingia kwenye ardhi ya nchi ya Ukerewe na kujichimbia chini kwenye udongo. Na Mpuluko bin Mzee Makene wa Kisolya akaendelea kupigilia huo umambo mpaka ukashika hasa na kuwa kama mti mwingine ulioota kando ya mti wa mbulumatale.” (JSW: 175)

Padre Alhaji Sheikh Joni Juma Profesa Simba-Mbiti aliteketeza uhai wa watu wengi sana kwa kisingizio cha kile alichokidai kukubuhu katika uganga wa mitishamba; hali kadhalika ali-watembea na wanawake wengi na kuwanajisi wanawali wengi wala idadi yao haijulikani. Mhusika huyu anafanana sana na mhusika Mwenyekiti Mtendaji Kanali Alhaji Muhamedi Nzoka Mwanakulanga kwa udhalimu, hujuma, ufuska, uroho wa utajiri wa haraka haraka kwa njia ya mauaji katika riwaya ya mwandishi huyohuyo Gabriel Ruhumbika, iitwayo *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992) (tz. tanbihi 2).

3.8. Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Dhamira ya nafasi ya mwanamke katika jamii inasawiriwa kupitia wahusika wakuu wawili Padre Joni na Bugonoka. Katika riwaya hii tunaona jinsi Padre Joni anavyowadhalilisha wanawake. Anawatumia wanawake kama vyombo ilimradi kukidhi uchu wake binafsi. Katika sura ya kumi tunasoma:

“Na huku huko kwake Mwanza amefuga zizi zima la mabinti za watu. Wanawake vijana na wazuri ajabu wa kila kabila na kila rangi [...] anaowaharibia maisha hao mabinti za watu, ikiwa ni kuwatumia kama chombo cha kutolea uchafu wa mkia wake tu, basi.” (JSW: 168)

Kabla ya kutoroka kutoka Dakar na kurejea Tanzania anashikishwa adabu na Maimuna kwa kumshikia jisu huku akiwa amewaalika wanawake watano wa nyumba jirani. Mikono ya wanawake hao watano ilimshikilia Padre Joni barabara kama amefungiwa kwa kamba ya nyuzi za chuma (tz. JSW: 134f.). Msomaji anaposoma hayo anaweza kukubaliana na hatua za kijasiri ambazo Maimuna alizichukua dhidi ya mumewe mwenye tabia zifafanazo na mbwa-koko.

Mhusika Bugonoka ndiye aliyekuwa mwanamke wa kwanza kumwadhibu Padre Joni alipomtaka kumbaka, alishikwa na ghadhabu na hivyo akamdhibiti:

“Padre Joni akatupwa nyuma kwa nguvu na miguu yake ikajigonga kwenye jiwe la kusagia nafaka, akaanguka chini akiwa chali, miguu juu, kiuno kwenye jiwe na kiwiliwili kikajipiga chini upande mwingine wa jiwa la kusagia.” (JSW: 96)

Ingawa Bugonoka alikuwa mwanamke shujaa mwenye sura nzuri, lakini alidumisha ubikira wake hadi alipouawa kikatili na mamluki wa Padre Joni ikiwa eti kulipiza kisasi kwa kumka-talia ngono badala yake alikikuta cha mtema kuni. Baada ya mauaji hayo ya kishirikina mganga Profesa Simba-Mbiti anapovipokea baadhi ya viungo vya siri vya Bugonoka anavitolea kejeli na kashfa:

“Na ukataka kuniua ati kwa kuthubutu kutamani hiyo bikira yako. Nimekuua, halafu nimejipatia hiyo bikira yako uliyoninyima. Ulinikatalia kufaidi ubikira wako ulipokuwa hai, ngoja sasa ndipo niufaidi hasa, kwa kuufanya dawa ya kunitajirisha na kunipatia pesa na sifa zitakazonipatia wanawake na wasichana wa kila aina hadi tani yangu!” (JSW: 149)

Licha ya kwamba Bugonoka aliuawa kikatili kwa mipango ya uchu wa utajiri wa padre-sheikh, huyo ni shujaa na mkombozi wa jamii nzima na hasa wanawake.

Dunia inapopiga vita kali dhidi ya gonjwa sugu la UKIMWI ambalo uambukizaji wake kwa asilimia nyingi hutokana na vitendo vya ngono, kumbe padre-sheikh ni kikwazo na hasimu mkuu kwa jamii.

4. Muundo na mtindo

Gabriel Ruhumbika amekuwa makini sana katika kutumia muundo rejeshi. Ameibua visa kadha wa kadha ambazo zinaleta taswira ya kuisimua na kumfanya msomaji apende kuendelea kukisoma kitabu ili kujua nini kinatokea baadaye kwa jinsi ya mfululizo wa mbinu tofauti za taharuki. Aidha, mtindo wake wa kuhusisha matukio ya kweli ya kihistoria na ambayo huleta kero kwa jamii, huwagusa kwa kina walengwa wake. Mandhari na wahusika anaowajenga huakisi uhalisia wa maisha ya jamii ya Tanzania na sehemu nyingi za Afrika. Ndumba, yaani kibuyu cha waganga wa kienyeji kinaelezea bayana mintarafu hilo janga sugu la wazawa.

Mtindo wake wa kusimulia kwa lugha ya picha kunamchukua msomaji hadi ughaibuni. Mfano mmoja ni ufuatao:

“Na mwezi wa ajabu huo ukang’aa mara moja tu na kufifia, na hapohapo ukawaka tena lakini kwa mwanga mwekundu, mwanga mwekundu kabisa, kama damu! Na hapohapo humo ziwani, dhoruba kali ikavuma, mawimbi makubwa ajabu yakapiga, na mtumbwi wao ukatoswa hadi juu kwenye kilele cha milima hiyo ya maji kabla ya kuteremka tena kasi kweli, kama kijiti kwenye maporomoko ya maji, hadi chini ziwani!” (JSW: 30)

Kumbe baada ya kurasa chache tu tunaelezwa taarifa tofauti kabisa na ndugu waliowasubiri nchi kavu:

“Hapakuwa na dhoruba usiku huo. Wala hapakuwa na mvua, au hata upepo mkali. Walipoteaje?” (JSW: 33)

Hiki kilikuwa ni kitendawili kinachodhihirisha umahiri wa mtindo wake wa pekee katika uandikaji fasihi.

Pia anatomia mtindo wa kumfanya mhusika anaongea na ndugu zake huko ahera, lakini angeweza kusema kwa mhusika alipokuwa amelala usingizi aliota ndoto na kuongea na marehemu ndugu zake:

Mama na Baba, mmeniona leo! Kazi yangu nimemaliza. Niko tayari sasa, siku yoyote kuja kujiunga nanyi. Nimemaliza kazi mliyoniachia. Mjukuu wenu nimemfikisha kwenye maisha tuliyokuja kumtafutia huku ugenini.” (JSW: 110)

JANGA SUGU LA WAZAWA: UCHAMBUZI NA UHAKIKI

Hisia kama hizo ameziibua mwandishi akimaanisha kifo cha mhusika kwa mantiki kwamba sasa anaweza kuonana na ndugu zake marehemu.

4.1. Matumizi ya Lugha

Hapana haja ya kuelezea jinsi vipi Ruhumbika anavyokimudu Kiswahili sanifu katika uimari-shaji wa tungo zake. Katika riwaya hii ametumia pia lugha nyingine mbalimbali: Kiingereza (*Middle School, pickup, sabbatical, Cambridge School Certificate, Africanisation, fresh*), Kitalini (*fratera, sacramento, In nomine Patris et Filii et Spiritus Sancti!*), Kikerewe (*ekome, epanza, lubigo, kisanzo, manselelya, mbozu, lugega, omukama, olumbwe, amasanga, abakama, ilumba*), na Kiarabu (*sheikh, alhaji*).

Aidha, ametumia fani mbalimbali za kifasihi ikiwa ni pamoja na nahau, misemo, methali na tamathali za semi.

Methali

Mwandishi anatumia methali katika sehemu kadhaa za matini. Mifano miwili ni hii:

“*Kipya kinyemi, ingawa kidonda!*” (JSW: 122)

“*Nyati wakipigana zinazoumia ni nyasi!*” (JSW: 170)

Tamathali za Semi

Tamathali za semi hutumiwa ili kutia nguvu na msisitizo katika maana na mtindo wa kazi ya fasihi. Riwaya hii imejaa aina nyingi za tamathali za semi. Ifuatayo ni mifano michache tu.

Tashibiha

Tamathali hii hutumika kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia viunganishi, kwa mfano *kama; mithili; mfano wa; kana kwamba*, na vinginevyo. Mfano mmoja ni “*...ngozi yake nyeusi laini kamaya mtoto mdogo*” (JSW: 15).

Sitiari

Hii ni tamathali ya usemi inayofanana na ile ya *tashibiha* ila haitumia viunganishi. Mfano:

“*...alikuwa sasa amefikisha watoto saba, lakini mpaka hapo alikuwa bado chuma hasa!*” (JSW: 130)

Mdokezo

Mdokezo ni tamathali ya usemi ambayo huanza kusema kauli bila ya kumalizia ilimradi wengine wamalizie. Mifano miwili ni “*sharti awe...*” (JSW: 15) na “*T’m...noko!*” (JSW: 101).

Tanakali Sauti

Hii ni tamathali ya usemi inayoiga sauti ya mtu, kitu, mnyama au mlio/mshindo wa kitendo kiwacho katika kazi ya sanaa. Mifano ya tanakali sauti ni ifuatayo: “*Myee!*” (JSW: 32); “*Mbum!*”; “*Wooo! Wooo! Wooo!*” (96); “*Hiriririi! Hiriririi! Hiriririi!*” (105); “*Puuu!*” (147); “*Pwaa!*” (148).

Takriri

Takriri ni usemi unaorudiarudia neno, maneno, muundo, kauli, sentensi, au vipengele vingine.

“*Ng’ombembogo akapotea hivi hivi, mchana mchana, kwenye maji mafupi!*” (JSW: 54)

“*[...] na akanenepa na kunenepeana*” (JSW: 131)

Dhahaka/Kejeli

Tamathali hii hubeza, hudharau, hubeua, huumbua, hukashifu, hufedhehesha, husuta, hukufuru, huponda, hulaumu na kulaani.

“*Baba! Padre Joni, huyu mwanamke ni mbaya wako kweli. Karibu apasue nglopu za ugusha wako! Na bila hizo nglopu, Baba, naamini mimi, mwenge wako hauwaki. Hao wanawake unaowapenda sana hivi ungabakia wawangalia kama huwaoni!*” (Kiswahili chenye lahaja ya Kisukuma; JSW: 100)

4.2 Upeo na Falsafa

Mwandishi anadokeza matatizo yanayoikabili jamii na kuyatafutia suluhisho. Kwa mfano, Bugonoka aliongea na wazazi wake Mzee Ninalwo na Bibi Nakazenze:

“*Mimi sikubali kwamba Mungu huyo mmoja anaweza kuumba watu wote halafu akaamua kwamba dini zote za watu weusi ni za kishenzi na dini za kweli ni za watu weupe tu. Oia siamini kuwa hiyo dini ya kikristu na dini nyingine yoyote ile, ina weza kunifundisha kuwa mtu mwema kuliko mliyoyonifundisha nyinyi baba na mama, kutokana na maadili ya dini yetu na ya mababu zetu.*” (JSW: 77)

Ruhumbika anaitanabaisha jamii kuhusu uhalisia wa maisha ya binadamu:

“*Mtu kutimiza majukumu yake ndicho kipimo cha ubinadamu wake. Na ndiyo pia kuishi maisha yenye maana na kufa kifo kinachotakiwa.*” (JSW: 179)

Na kadiri biashara ya ushirikina ilivyoendelea kukua na kushamiri kwa waganga hao kudai ngozi au viungo vya binadamu ikaleta hofu kubwa kwa jamii ya Tanzania na mahali pengine katika bara la Afrika, mwandishi anatoa ajenda ya kipaumbele, hivyo haraka kuitishwe mkutano wa Umoja wa Afrika:

“*Tulikuwa tunaandaa mikakati na mbinu za kupiga vita janga sugu la wazawa wa nchi zote: ushirikina na madhara yake yote. Hyo vita itanza kote Barani Afrika mara moja na hakuna mkuu wa nchi ya Kiafrika atakayepumua katika kupiga vita huyo adui mkuu wa jamii yetu hadi ushindi kamili upatikane.*” (JSW: 192)

5. Hitimisho

Kwa jumla, riwaya hii ya *Janga Sugu la Wazawa* linaakisi hali halisi ya mfumo wa maisha ya Wakerewe kwa kuwalinganisha na jamii inayokizunguka kisiwa cha Ukerewe, mintarafu imani za jadi na jinsi Ukristo ulivyoathiri misingi hiyo. Hali kadhalika, riwaya hii linasisitiza umuhimu wa kuzingatia kuthamini tamaduni, mila na desturi na maadili mema katika jamii.

Kwa yamkini, ‘janga sugu la wazawa’ wa nchi zetu siyo jingine ila ushirikina na madhara yake ambalo halina budi kupewa kipaumbele zaidi na kupigwa vita kwa vitendo kwa nguvu za mshikamano wa jamii zote barani Afrika.

Marejeo

- Bertoncini-Zúbková, Elena. 1989. *An Outline of Swahili Literature*. Leiden: E. J. Brill.
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS). 1981. Dar es Salaam: TUKI.
- Kitereza, Aniceti. 1980 [1945]. *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. Ntulanalwo na Bulihwali*. Juzuu I&II. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Kitereza, Aniceti. 2002. *Mr Myombekere and His Wife Bugonoka. Their Son Ntulanalwo and Daughter Bulihwali: The Story of an Ancient African Community*. Translated from Kikerewe by Gabriel Ruhumbika. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- Ruhumbika, Gabriel. 1969. *Village in Uhuru*. Harlow & London: Longman.
- Ruhumbika, Gabriel. 1974. *Towards Ujamaa. Socio-political Essays on the Development of Tanzania*. Dar es Salaam-Nairobi-Kampala: East African Literature Bureau.
- Ruhumbika, Gabriel. 1974. *Parapanda. Wali wa Ndevu na Hadithi Nyingine*. Dar es Salaam-Nairobi-Kampala: East African Literature Bureau.
- Ruhumbika, Gabriel. 1976. *Afrika Inakwenda Kombo*. Dar es Salaam, Nairobi, Kampala: East African Literature Bureau. [Tafsiri ya René Dumont, *L’Afrique noire est mal partie*, Paris: Seuil, 1963.]
- Ruhumbika, Gabriel & Clement Maganga. 1978. *Viumbe Waliolaaniwa*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House. [Tafsiri ya Frantz Fanon, *Les damnés de la terre*, Paris: Editions Maspéro, 1961.]
- Ruhumbika, Gabriel. ²1981 [1978]. *Uwike Usiwike Kutakucha*. Arusha & Dar es Salaam: Eastern Africa Publications Limited.
- Ruhumbika, Gabriel. ²1995 [1992]. *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House. [Chapa ya kwanza: Economic Research Bureau, University of Dar es Salaam.]
- Ruhumbika, Gabriel. 2002. *Janga Sugu la Wazawa*. Dar es Salaam: E & D Publishers Ltd.